

This booklet on Becoming a Parent was developed by the Tanzania Home Economics Association with support from Our Bodies Ourselves. Other booklets and more information on the project are available at <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

MACHAGUO YA UZAZI

KUFIKIRIA KUWA MZAZI

Nusu ya mwisho ya karne ya 20 ilishuhudia mabadiliko makubwa mno katika uamuzi wa wanawake kuwa wazazi. Katika kipindi cha mabibi wa mabibi zetu, kukosekana kwa njia za kupanga uzazi zenye ufanisi, pamoja na matakwa ya mila za kijamii, kulimaanisha kwamba wanawake wote wenye uwezo wa kubeba ujauzito walikuwa na watoto. Leo hii, hata hivyo, kuna machaguo mengi zaidi. Ufahamu zaidi wa uzazi wa majira, kuruhusiwa kutoa mimba kisheria, na teknolojia za kisasa za katika uzazi vinatoa mwanya kwa wengi wetu kuweza kuzuia na kuamua wakati upi wa kupata watoto. Zaidi ya hapo, kubadilika kwa sheria na desturi za kijamii kumpelekea kukubalika zaidi kwa waawake ambao wanaamua kutokuwa na watoto, pamoja na wale walioamua kuishi bila wenzi, wenye wenzi wa jinsia moja, na aina nyingine nyingi za familia ambazo hazijazoeleka kwenye jamii ambazo zinataka kupata au kuasili mtoto.

Baadhi yetu tumekuwa na wazo la kupata watoto siku zote, wakati wengine tunafahamu fika kuwa hatutaraji kabisa kuwa na watoto. Kuna kipindi wengi wetu hujikuta tukipambana na hisia kinzani. Aghalabu uhalisia wa maisha hupunguza kwa kiasi kikubwa machaguo yaliyopo: Unaweza kuwa na pesa na rasilimali nyingine kidogo sana kiasi kwamba ukashindwa hata kuwazia ni kwa namna gani utaweza kumtunza mtoto. Unaweza kuwa mseja na hauko tayari kumlea mtoto peke yako, au ukajikuta una ujauzito na hivyo kulea mtoto kinyume na uamuzi wako. Unaweza kuwa mgumba, au una ugonjwa au kilema hivyo kushindwa kubeba mimba, kukaa na ujauzito, au kuwa mzazi. Lakini bado, kuweza kuwa na uwezo wa kudhibiti uwezo wetu wa kupata mimba kunaweza kutupa muda wa kufikiria kwa umakini juu ya uamuzi wa kuwa mzazi.

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi ("Becoming a Parent"). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

Sehemu ya kwanza ya sura hii inatazama baadhi ya maswali unayotakiwa kujiuliza endapo unafikiria kuwa mzazi. Inatoa nyenzo za kukusaidia katika mchakato huu. Kama umeamua kupata mtoto, maswali mengi zaidi ambayo mabibi zetu hawakuwahi kujiuliza: Niendelee na nia yangu ya kutaka kupata ujauzito? Niasili mtoto, au niwe mzazi wa kufikia? Sehemu ya pili ya syrah ii inayatazama kwa undani masuala haya.

KUFANYA UAMUZI

KUWA MZAZI KATIKA DUNIA YA SASA

Kama ilivyo kwa maamuzi mengine binafsi tunaoyafanya, uamuzi wa kupata mtoto hushawishiwa na familia zetu, utamaduni na jamii tunamoishi. Jamii ya kimarekani inaamini kwamba kuwa mama ni kitu cha muhimu sana katika utambulisho na mafanikio ya mwanamke, lakini bado serikali yetu haitoi msaada wa kutosha kwa watoto na familia zao. Tofauti na zilivyo nchi nyingine zilizoendelea, nchi ya Marekani haitoi malipo ya mapumziko ya kifamilia, wala huduma ya uhakika ya afya kwa raia wake, na huduma ya afya yenye ubora wa hali ya juu ni ghali sana.

Zaidi ya hapo, mtazamo wa mama “mzuri”/mama “mbaya” bado ni mojawapo ya mada kuu ya mijadala kwenye jamii, na unachangia sana kuamua namna mzazi atakavyochukuliwa kwenye jamii. Vyombo vya habari vimesheheni masimulizi kuhusu “ushindani” uliopo kati ya wanawake “wanaochagua” kuwa “wazazi wa muda wote” (wakinamama wanaoshinda nyumbani) na wale “wanaochagua” kufanya kazi za kulipwa (wakinamama wafanyakazi). Mtazamo huu unaweza kutufanya tuamini kuwa wanawake wote huangukia katika kundi moja au lingine, huku kila kundi likiwa na mtazamo hasi juu ya lingine. Kile kinachoweza kuitwa “Masimulizi ya Mita vya Kinamama” kinatualika tuchague upande wa kuunga mkono, kuwasifia kinamama wanaofanya kazi kwa kuweza kujigawa kati ya kazi na familia au kuwashutumu kwa “kuwatelekeza” watoto wao; kuwasifia kinamama wanaokaa majumbani kwa kuweza kujitolea kiasi hicho kwa watoto wao au

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see:
<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

kuwalaumu kwa kuuchukulia utambulisho wao kama wanawake kumaanisha uzazi pekee.

Lakini ukweli ni kwamba, maisha ya wanawake wachache sana yanaweza kugawanywa kwa namna hii. Kwa mujibu wa ripoti ya sensa ya Marekani kwa mwaka 2002 zaidi ya asilimia 50 ya wanawake wenye watoto wachanga na silimia 72 ya wanawake wengine walikuwa wanafanya kazi. Wanawake wengi wenye watoto wadogo wanafanya kazi kwa muda wa ziada, au husubiri mpaka watoto wao waanza shule kabla ya kurudi makazini. Wakinamama wengi huingia na kutoka kwenye kazi za muda wote na zile za muda wa ziada kulingana na mahitaji ya kifamilia. Uhalisia ni kwamba wengi wetu hatuna budi kufanya kazi, iwe tunapenda au la. Uhalisia huu unawagusa hasa kinamama wasio na wenzi, ambao idadi yao kwa sasa inafikia milioni kumi nchini Marekani.

Kwa kiasi kikubwa, mambo yanayowakabili kinamama hayamulikwi sana na vyombo vya habari wa kipekee na hayajumuishwi ipasavyo kwenye sera za umma. Kwa mfano, wakati wa kipindi cha “mabadiliko ya huduma za jamii” kwenye miaka ya 1990, vyombo vya habari vilijaa kila aina ya habari mbaya kuhusu wakinamama ambao walikuwa wakifaidika na huduma za ustawi wa jamii kwa miaka mingi, habari ambazo haziwezi kuelezewa kutoka katika mtazamo wa wanawake hawa. Makala zilizosheheni habari juu ya mwanamke wa “kawaida” aliye katika mpango wa ustawi wa jamii, aitwaye Denise M au Letitia B., ambaye ni mama wa watoto watano kutoka kwa wanaume wane tofauti¹ na anayetumia siku zake zote akivuta sigara na akiwa hafanyi jitihada zinazoeleweka za kutimiza mahitaji ya watoto wake ambao bado ni wadogo. Licha ya ukweli kwamba wengi wa wanaonufaika na huduma hizi ni watu weupe, siku karibu zote alikuwa ni mwanamke wa mbari nyingine, aghalabu Mmarekani mweusi, ambaye alionekana kama “mama mbaya.” Kurudiwa rudiwa kwa habari kama hizi kuliwahamasisha wasomaji au watazamaji kujenga uhusiano kati ya mbari na umasikini, na kutokuwajibika kwa mama, na kuwawajibisha kinamama walio na uhitaji kwa kwa kushindwa kuwapatia watoto wetu mahitaji mbalimbali. Katika kipindi cha miaka hiyohiyo, “mabadiliko ya huduma za jamii” yaliondoa kabisa mtandao wa msaada wa kifedha na kijamii

¹ Ukweli ni kwamba, mwanamke wa kawaida aliye katika mpango wa huduma za ustawi wa jamii ana watoto chini ya watatu.

ambao ulikuwepo ka muda wa miaka sitini. Ujumbe kwa wanawake ulikuwa wazi: Linapokuja suala la watoto, uko peke yako.

Tamaduni zetu zinaonyesha baadhi ya kinamama kama waliokamilika, wengine kama wabaya, na inachukulia “kazi” ya kuwa mama kama ya mchezo tu. Wakinamama wengi hushtukizwa wakiwa hawajajiandaa na pengo kubwa kati ya kufikiria uzuri wa kuwa mama na uhalisia wa kila siku wa kuwapatia watoto upendo, mazingira mazuri ya kukulia na kuwajali.

KULIFIKIRIA SUALA HILI KWA UNDANI

Ina maana gani kuwa mama katika dunia ya kisasa? Itamaanisha nini kwangu kama nitakuwa mama? Haishangazi sana kuona kila swali halina jibu la moja kwa moja au linalokubaliwa na wote.

Ninasikia mitazamo miwili inayopingana. Mmoja, inaogofya kuwa mama; mwingine, utajutia kuwa mama; maisha yako yatabadilika.”

Nilipata mtoto nilipokuwa na umri wa miaka 46. Kabla ya hapo, ingawa nilikuwa napenda kuwa na watoto wa watu wengine, muda wowote lazima kuna kitu kibaya kilitokea na mtoto akaanza kunikera, nilifikiria mwenyewe moyoni, Ningewezaje kumudu majukumu ya kuwa mama kwa muda wote? Kwa kiasi fulani, kuwa mama kulibadilisha fikra hii. Kuna muunganiko wa kipekee usioweza kuelezeka – wa asili kabisa kwenye uhusiano, ambao baada ya muda mrefu unameza kabisa kero ndogo ndogo zinazotokea kila siku.

Napenda watoto, lakini sijawahi kuwa na msukumo mkubwa wa kuwapata mimi mwenyewe. Siku zote Jinsi gani nimekuwa nashangaa: unawezaje kustahimili mikiki mikiki ya kujijali mwenyewe na kuwa mzazi? Kwa kipindi kirefu cha miaka yangu kati ya 30 na 40 nilikuwa pekee bila mwenzi, na baadaye nilianzisha uhusiano na mwanamme ambaye alikuwa na uhakika kabisa kwamba hakutaka watoto. Lakini bado nilihisi kuwa ilikuwa muhimu kwangu kufanya uamuzi wa busara kwa ajili ya maisha yangu – Sikutaka kusema hapana kwa sababu tu yeye alisema hapana. Nilizungumza na wanawake wengi, na kutazama kila upande, halafu nikachukua uamuzi wa kutokuwa na mtoto. Ugumu ulikuja pale nilipotakiwa kuwaambia wazazi wangu, kwa sababu nilijua watasikitishwa sana na uamuzi

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see:

<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

wangu. Lakini nilipofanya kitendo hiki nilijisikia nafuu, na ukweli ni kwamba, sikufikiria sana juu jambo hili tangu kipindi hicho.

Kadiri unapokuwa unakaribia kufika uamuzi wako, ni busara kulitazama suala hili kwa kina. Watoto wanavutia, werevu, na wanafurahisha. Wanaweza kutufundisha mambo mengi kadiri wanavyokua na kubadilika inasaidia kuangalia kila upande wa swala hilo, watoto hujishughulisha, wabunifu, moyo wa kupenda kufanya vitu fulani fulani na ni wachekekehaji. Wanaweza kutufundisha mengi wakati wanapokua na kubadilika; tunakua na kubadilika pamoja nao. Wanatupa changamoto na kututia moyo wa kuifanya dunia kuwa pahali bora pa kuishi, na wanatuwezesha kuwa sehemu mwendelezo wa maisha ya kila siku. Wengi wetu hupenda kuwalea na kuwapenda watoto wetu wenyewe, kuipata ile furaha ya kipekee inayotokana na kuwa mama.

Kwa wakati huo huo, kuwa mzazi kunajumuisha kubadilisha hali ya hiari na uhibititi katika matendo yetu ya kila siku, kwa jukumu kubwa, ratiba zinazotubana sana, pamoja na vurumai kwenye maisha yetu ya kila siku. Unaweza usifurahie ile hali ya kuwa na watoto kila siku; Unaweza kuwapenda bila ya wewe mwenyewe kutaka kuwa na wa kwako. Unaweza kuhofia kualeta watoto katika dunia hii yenye matatizo kibao au unaweza kuwa unataka kutimiza ndoto zako ambazo haziendani na kulea watoto. Kutokuwa na watoto mara nyingi humaanisha kuwa huru zaidi na muda, nguvu, na pesa zaidi kuwekeza kwenye mahusiano, kazi, na vitu vingine vipendavyo.

Wengi wetu tunawazia kwa jinsi gani uamuzi huu utaathiri maisha na mahusiano yetu. Kama una mwenzi unaweza kuhofia kuwa mtoto anaweza kuubadilisha, kuletea matatizo au hata kuudhofisha uhusiano wako. Kuwa na watoto kunaweza kuvuruga mipango yako ya kujiendeleza kitaaluma, kiuchumi, au kiweledi. Mwenzi wako au watu wengine wanaweza kukushinikiza kupata mtoto hata kama wewe mwenyewe hautaki au hauko tayari. Kwa upande mwingine, unaweza kuwa unahofia kuwa kuiachia fursa ya kuwa mama ipite ni kujikosesha bahati ya kipekee maishani mwako.

Maswali mengi hujitokeza. Mengine yana majibu ya moja kwa moja; mengine ni magumu sana: Je kazi yangu inaniimarisha kifedha? Je, nina nyumba isiyotetereka? Je, mwenzi wang au mtu mwingine yeyote wa nyumbani kwangu ni mkatili? Vipi kuhusu pombe na dawa za kulevya katika maisha yangu? Je kuna

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi ("Becoming a Parent"). For more information, see:
<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

matatizo ya kiafya kwenye familia ambayo yanaweza kuwa ni ya kurithi? Je, nina mbinu zinazohitajika kuwa mzazi mzuri? Au niko tayari kujifunza mbinu hizo? Nitawezaje kujigawa kati ya kazi na kutunza watoto? Kama sina mwenza, ni kwa kiasi gani kuwa na mtoto kutaathiri mahusiano yangu yoyote mapya nitakayoyaanza? Je, nina bima ya afya ya kutosha na ninaweza kupata huduma nzuri ya afya? Vipi kuhusu gharama za kifedha? Maadili gani ningependa kumfunza mwanangu, na ni nani atanisaidia kufanya hili? Kwenye jamii ya aina gani ningependa mwanangu akulie? Je, nitapata msaada pale mimi au mwanangu tutakapopata ulemavu? Je, niko tayari kumwandaa mwanangu kukabiliana na changamoto za kimaisha, kama vile ubaguzi wa rangi na kijinsia, na chuki dhidi mahusiano ya jinsia moja?

Kama una patna, zungumza naye juu ya aina ya na kiasi cha majukumu kila mmoja wenu atakuwa tayari kuchukua katika kumlea mtoto. Je, mmoja wenu atakaa nyumbani na mtoto? Au mtatfuta mwangalizi wa mtoto? Ikiwa patna wako ni mwanamume, unaweza kuhitajika kuwa mwangalifu uapozungumzia suala la yeye pia, na sio wewe tu, atakavyougawa muda wake kwa ajili ya kumwangelia mtoto, majukumu ya kazi, na kufanya mabo mengine ya muhimu.

Jaribu pia kutathmini juu ya uwezo wako kihisia katika kumtunza mtoto. Je, unaishi na watu wanaojali kwa dhati watakaoweza kukusaidia kubaki na mtazamo, na tabia yako, ucheshi, na uwezo wako wa kufanya maamuzi utakapokuwa kwenye mabadiliko na kipindi kigumu kihisia ambacho hutokea kwa wazazi wote? Kadiri unavyofikiria ikiwa unataka kuwa na mtoto au la, weka akilini kuwa kuna kipindi kitafika utajutia na kutamani kuwa ulifanya uamuzi tofauti na uliufanya.

Kupata mtoto ni uamuzi usioweza kubadilishwa. Utabakia kuwa mzazi maisha yako yote. Hata kama tutaamua kuwatoa watoto wetu waasiliwe na watu wengine bado tutaendelea kuwakumbuka kwa namna mbalimbali. Lakini kama utaamua kutopata mtoto katika kipindi fulani cha maisha yako, uamuzi utakaoufanya muda huo sio lazima uwe uamuzi wa mwisho. Na endapo umeshapitisha umri wa kuweza kuzaa, bado una nafasi ya kuasili, kuwa mzazi wa kufikia, au, katika uhusiano mpya, kuwa mzazi wa kambo. Muda wowote ule, unaweza kuwafurahia watoto wanaokuwa sehemu ya maisha yako.

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi ("Becoming a Parent"). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

IKIWA UNA KUMBUKUMBU MBAYA ZA UTOTONI...

Wanawake ambao walipitia kipindi kigumu wakati wa utotoni wanaweza kuwa na wakati mgumu pia katika kufanya maamuzi juu ya kupata mtoto au la. Endapo unajisikia kukoseshwa amani au kuumizwa na kumbukumbu za mambo yaliyotokea kipindi ukiwa mdogo, unaweza ukajiuliza kama utweza kweli kumtunza mtoto. Wanawake wengi ambao walilazimishwa kujamiiana na ndugu zao wa karibu au kunyanyaswa kijinsia mara nyingi huhofia mabadiliko ya kimwili yanayoletwa na ujauzito, na kufanyiwa vipimo na daktari au kufanyiwa uhimilishaji kunaweza kuwafanya wajisikie kama wanavamiwa undani wao. Baadhi ya wanawake waliopitia vitendo kama hivi huona ujauzito na kujifungua kama vitu vinavyowaibulia tena kumbukumbu hizi mbaya au hisia za udhaifu na kutokuwa na usaidizi wowote.

Mara nyingi huwa si rahisi kufikia uamuzi wa kupata mtoto mpaka pale utakapokuwa umeweka sawa kila kitu kinachokutatiza akilini mwako. Kupata ushauri nasaha kunaweza kukusaidia kuondoa kumbukumbu mbaya za nyuma na kukupa nafasi ya kuweza kuufikiria vizuri uamuzi wa kuwa na mtoto. Baadhi ya vituo vya kutoa ushauri nasaha vya kutetea na kupigania haki na usawa kwa wanawake, mawakala wa huduma za familia, vituo vya afya ya jamii, na mashirika mengine ya kijamii wanatoa msaada wa kitaalamu bure au kwa gharama nafuu sana.

Ni vigumu kupata neno sahihi kuelezea kutokuwa na mtoto. Watu wengi wanatumia “asiye na familia”. Sura hii pia inatumia usemi huu, ingawa unasahau njia mbalimbali ambazo watoto – na kujitolea kwa ajili ya watoto – wanaweza kuyagusa maisha yetu hata kama sisi sio wazazi wao.

UWEZO WA KUZAA NA KUEEKA

Vyombo yva habari vimejaa hadithi za kuogofya kuhusu wanawake na hatari mbalimbali za kibaiolojia tulizonazo. Lakini hadithi hizi zinatakiwa kupembuliwa kwa umakini kabla ya kuzikubali kama zilivyo. Uwezo wa kupata mimba hupungua kadiri umri wa mwanamke unavyoongezeka. Lakini kupungua huku kwa uwezo huu kunapoanza, na kiwango cha kuongezeka kwake kunatofautiana sana.

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see:

<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

Wakati ni muhimu kupata taarifa sahihi kuhusu nafasi za mwanamke wa kawaida za kupata na kubeba ujauzito kulingana na umri tofauti, ukweli kwamba wanawake wengi hupoteza uwezo huu wa kupata ujauzito wakiwa na miaka thelathini na nane kuliko iliyo wakiwa na miaka ishirini na mbili unatakiwa uwe kichwani mwako unapoamua kuchukua uamuzi wa kupata mtoto au la. (Kwa maelezo zaidi, tazama “Uwezo wa kupata Ujauzito na Kuongezeka kwa Umri” kwenye tovuti, www.ourbodiesourselves.org.)

MIONGOZO YA KUFANYA MAAMUZI

Kufanya maamuzi wakati mwingine huwa ni rahisi unapokuwa unaelewa kuwa:

- Kuchagua kuunamaanisha kuachana na machaguo mengine.
- Utahitaji muda wa kufikia uamuzi ambao ni wako mwenyewe, na ambao unadhani utakufanya uwe na furaha.
- Huwezi kuwa na uhakika kwa asilimia 100.
- Uamuzi “mbaya” hautaharibu maisha yako.
- Ni muhimu kutumia mantiki na uwezo wako wa kuhisi jeme na baya unapokuwa unafikiria machaguo yako.
- Uweza kutafuta msaada wa familia na marafiki.
- Unaweza kufikiria machaguo ambayo hayajazoeleka ya kulea watoto.

(Kwa majadiliano zaidi juu ya masuala haya, tazama “Miongozo ya Kufanya – Maamuzi” [W39] kwenye tovuti, www.ourbodiesourselves.org.)

CHANGAMOTO ZA KAWAIDA KWA WOTE

Kuamua (na wakati upi) kupata mtoto au watoto ni uamuzi wa muhimu, lakini bado wengi wetu tunaucheleweshwa, tunaukataa, au kuuepuka kabisa. Zifuatazo ni baadhi ya changamoto na mambo yasiyo ya kweli.

1. *Kuepuka kuuacha uanuzi ujifanye wenyewe.* Baadhi ya wanawake huacha mambo yajiweke sawa yenyewe kwa kutotumia kinga yoyote ya mamba.

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see:
<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

Wengine huchelewa kufanya uamuzi kwa muda mrefu sana kiasi kwamba uamuzi huwa tayari umeshafanywa baada ya muda fulani.

2. *Kumwacha mwenzi wako kukufanyia uamuzi.* Yeye anaweza kuwa anapenda kuwa na mtoto au anaweza kukutaka umuahidi kuwa hautopata mtoto. Unaweza kuvumilia maamuzi kama haya ikiwa unaogopa kuwa mwenzi wako atakasirika au kuacha, au kama hauna uhakika na kutaka uamuzi huo ufanyike na umalizane kabisa na suala la kuamua. Kwa siku za mwanzoni za kuwa kwenye mapenzi, unaweza kukubaliana na matakwa ya mpenzi mwenzi wako ya kupata motto pamoja, halafu baadaye ukaja kuujutia uamuzi huo. Ni muhimu sana uwe na sauti katika kila uamuzi mnaoufanya pamoja.
3. *Kufikiria kuwa mwenzi wako atabadirika.* Kutokana na hamu yako ya kutengeneza familia, unaweza ukadharau dalili za tahadhari kwamba mwenzi wako anaonyesha kutokuwa tayari kuwa mzazi. Kama ana tatizo la kutumia dawa za kulevya au pombe, au ni mgomvi na mkali, si rahisi kabisa kwa yeye kubadilika hata pale mtoto atakapokuwa amezaliwa. .
4. *Kufikiria kuwa ni uamuzi wa kutokuwa na mtoto kabisa au kuwa na watoto wawili.* Wengi wetu tunadahni kuwa ni lazima tuwe na watoto wawili, ili mtoto wa kwanza aweze kupata mtu wa kucheza naye na pia kama sababu ya kuepuka kumdekeza mtoto wa kwanza. Hata hivyo, hakuna watoto wanaodeka, wapweke au wasioweza kuishi kulingana na mazingira kama watoto wenye ndugu wengine wa kuzaliwa tumbo moja. Kwa wengi mtoto mmoja anatosha kabisa.
5. *Kufanya maamuzi bila kufahamu hasa watoto wakoje.* Huwa unajisikiaje unapokuwa na watoto, hasa watoto wachanga? Kutumia muda kuwa nao pamoja ni moja kati ya mambo bora zaidi unayoweza kuyafanya. Jitahidi kuwafahamu kiundani watoto wa marafiki zako, mabinamu na wapwa pia. Wachukue na uende nao kutembea. Pitisha nao usiku hata mmoja mkiwa sehemu mbali na nyumbani. Tumieni muda wa mchana mkiwa kwenye viwanja vya michezo. Unajisikiaje? Unajisikia kuvutiwa nao?

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi ("Becoming a Parent"). For more information, see:
<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

6. *Kuwa na wasiwasi kwamba hutakuwa mzazi mwema.* Kwa sababu ya makosa yako unayoyaonyesha wewe kama mzazi, au tabia yako, utaweza kuwa na mashaka na uwezo wa kuweza kuwa mzazi. Kaa ukifahamu kuwa unaweza kujifunza, kuboresha matendo yako na kubadilika kwa kuongea na watu walio na msaada katika maisha yako., kusoma vitabu vinavyoelezea maswala ya kuwa mzazi au kuhudhuria masomo ya wazazi au kupata ushauri nasaha.

ENDAPO MNASHINDWA KUKUBALIANA NA MWENZI WAKO

Usiwe na hofu itakapoonekana kuwa wewe na mwenzi wako mnataka vitu tofauti. Wote mnahitaji muda wa kusikilizana na kutatua tofauti zenu.

Katika kipindi cha kutokuelewana juu ya jambo fulani la muhimu, ni rahisi kumwona mpenzi wako kama kikwazo kikubwa kwa mambo yako uliyoyapanga. Inaweza kuwa vigumu kusikiliza anachosema. Lakini kama utaweza kujishusha na kumsikiliza, na kujaribu kutolazimisha matwakwa yako, mnaweza kupata suluhu itakayowasaidia wote wawili.

Hizi hapa ni baadhi ya hatua zinazoweza kuwasaidia kufikia uamuzi wa pamoja:

- Kwanza, mpe nafasi mwenzi wako aeleze mawazo na hisia zake ili uweze kuelewa vizuri vitu gani vitakwamisha matakwa a mtazamo wako.
- Fikirieni kwa makini mambo mnayoweza kuyafanya. Kwa mfano, kama mmoja wenu anahofia kuwa ataelemwa na majukumu, mnaweza kujadiliana juu juu ya kuwa na mtoto mmoja pekee, au kuangalia kama kuna uwezekano wa familia na ndugu zenu kujitolea kuwasaidia. Kwa upande mwingine kabisa, endapo mwenzi wako hayuko tayari kukosa nafasi ya kuwa karibu na watoto, tafuteni namna ya kuweza kuwa pamoja na mabinamu au wapwa zenu, au kufanya kazi za kujitolea kwa watoto.

Sharti muhimu la kwanza katika kuwasiliana ni kwamba wote mkubali kueleza hisia, mawazo na mambo mnayoyataka na msiyoyataka. Uwazi huu utakufanya usijifunge kwa namna ambayo utashindwa kuelezea hofu, dukuduku na vitu ambavyo hauvifurahii. Baada ya kufanya hivyo, ikiwa mmoja wenu atajikuta akilazimika kuvumilia uamuzi ambao hakuupenda kwa asilimia mia, itabidi

afahamu kuwa alifanya juhudi zake zote kuheshimu mahitaji na matakwa ya mwenzake.

Kufahamu muda muafaka kunaweza pia kuwa suala la muhimu sana. Mmoja wenu anaweza kuwa anataka kumaliza shule au mafunzo ya kikazi kwanza, kuweka akiba ya kutosha kwanza, kuhamia kwenye nyumba nzuri zaidi, au kuendelea kupata ushauri akiwa peke yake au mkiwa wote wawili. Pengine mnaweza kuweka umakini katika kujadiliana juu ya kutambua muda muafaka kuliko hata uamuzi wenyewe.

Msimamo wa kila mmoja wenu unaweza kugongana na wa mwenzake juu ya namna ya kuwafunza adabu watoto, nafasi ya dini katika maisha ya mtoto, kuweka akiba kwa ajili ya elimu na maisha ya baadaye ya mtoto, ubatizo, kumtahiri, na mambo kama hayo. Kaa ukifahamu kuwa hata misimamo migumu kiasi gani huweza kubadilika baada ya muda fulani. Unaweza kuwaomba wanafamilia au marafiki unaowaamini wakusaidie kutatua masuala ya haya. Semina kuhusu uzazi, miongozo ya kiroho, washauri wa matumizi ya kifedha, na wataalamu wa matibabu ya kisaikolojia wanaweza kukusaidia pia.

Kama bado hamjapata ufumbuzibaada ya wiki au miezi kadhaa, mnaweza kuhitajika kuhudhuria vipindi maalumu vya ushauri kwa mtaalamu wa tiba aliyebobea katika masuala ya kutatua matatizo ya muda mfupi yahasuyo uzazi. Maamuzi yanayohusu uzazi ni magumu na mara nyingine yanaogopesha kufanya, lakini yanaweza pia kuweka wazi vitu gani ni vya muhimu kwako, na kukusaidia kutambua kitu unachohitaji na kukithamini zaidi.

KAMA UKIAAMUA KUTOPATA MTOTO

Baada ya mimi na mume wangu kuwa tumeoana kwa muda wa miaka michache, kulikuwa na maswali yasiyoisha juu ya lini tutaanzisha familia – hasa kutoka kwa wazazi, ambao rafiki zao wote walikuwa wana wajukuu. Kwa hiyo, kulikuwa na msukumo wa ziada wakati pale rafiki zetu wote walikuwa wameshapata watoto – hii ilibadilisha kabisa mwenendo wa urafiki wetu na yalikuwa na matokeo ambayo hatukuwa tumeyatarajia ya kuamua kutopata watoto.

Misukumo kutoka kwa jamii ya kupata watoto inaweza kuwa na nguvu ya kipekee. Kwa wale miongoni mwetu ambao tumechagua kutopata watoto mara nyingi

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see:

<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

hulaumiwa na wale wanaotuzunguka. Wengi wetu hugundua kwamba kujiunga na kundi la msaada au kutafuta njia nyingine za kuunganika na watu ambao wanaunga mkono na kufahamu uhalali wa uchaguzi wetu kunaweza kusaidia. (Kwa maelezo zaidi juu ya kuamua kutikuwa na watoto, tazama “Msaada.”)

KUFIKIRIA KWA KULINGANISHA

Njia moja ya kufikiria juu ya kufanya uamuzi huu ni kuangalia kwa namna gani maisha yako ya kila siku yanaweza kubadilika. Tenganisha karatasi katika safu mbili. Kwenye safu ya kwanza, onyesha ni saa mangapi kwa wiki unatumia katika shughuli zako za sasa, na kwenye ya pili, muda ambao unaweza kuutumia ikiwa ungekuwa na mtoto.

- Kazi
- Starehe/Burudani na kujumuika na watu
- Kupumzika, kwa mfano, kufanya yoga, kutaamuli
- Michezo
- Shughuli za kisiasa
- Shughuli za kidini
- Muda wa kuwa faragha na mwenzi wako
- Kulala

Je uko tayari kubadilisha utaratibu wako juu ya mambo haya au njia nyingine nyingi zisizohesabika usizozitarajia? Kama matarajio ya malengo hayo yanaonekana makubwa kuliko uwezo wako au hayawezekani kabisa, pengine si busara kuwa na mtoto kwa wakati huo.

NJIA HADI KUWA MZAZI

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

Tunapokuwa wazazi, huwa tunaianza safari ya mabadiliko. Kuwakaribisha watoto katika maisha yetu huleta nyakati za furaha, hofu, huzuni, na kukata tamaa. Kipengele hiki kinapitia kwa ufupi njia kadhaa tofauti katika kuelekea kuwa mzazi; kutungwa kwa mimba na kuzaa mtoto, kuasili mtoto, au kumlea mtoto wa kufikia.

KUBEBA UJAUZITO

UFAHAMU WA UWEZO WA KUSHIKA MIMBA / KUWEKA KUMBUKUMBU YA MZUNGUKO WAKO WA HEDHI KATIKA CHATI

Inashangaza sana kuona ni kiasi kidogo tu cha elimu juu ya miili yetu tunapatiwa kwenye vipindi vya afya mashuleni. Tunafundishwa mambo machache tu ya msingi juu ya uzazi wa majira, na ndiyo basi. Iko wapi taarifa ya kina juu ya kuweza kutabiri muda sahihi wa kupevuka kwa mayai ya uzazi na kujifunza jinsi ya kusimamia uwezo wako wa kipekee wa kupata ujauzito? Kwa hakika, mambo haya hayakuwemo kwenye topiki nilizofundishwa wakati niko sekondari..

Mara utakapoamua kujaribu kupata mimba, unaweza ukashangaa kujikuta kwamba unajua mengi sana kuhusu kuzuia mimba kuliko kuipata. Kuandika mzunguko wa siku za hedhi ni njia yenye manufaa katika kujifunza juu ya dalili za uwezo wa kushika mamba, na kuboresha uwezo wako wa kupata ujauzito. (Kufahamu zaidi, tazama Sura ya 13, “Anatomia ya Kimapenzi, Uzazi na Mzunguko wa Hedhi.”)

KUJITUNZA MWENYEWWE WAKATI UNAPOJARIBU KUTAKA KUBEBA MIMBA

Wakati unapojaribu kubeba mimba, unatakiwa kujitunza vizuri: Kula chakula bora, fanya mazoezi, na epuka kugusana au kukaa maeneo yenye vitu vya sumu. Wataalamu wengi wa afya wanashauri kutumia dawa za vitamini kabla ya kujifungua (hususan **follic acid**) na kuacha kuvuta sigara au kunywa pombe. Wengi wetu hubeba mimba moja kwa moja bila tatizo lolote. Wengine hulazimika kupitia mlolongo mrefu kidogo wa kushika mamba: wiki mbili za kusubiria yai kupevuka, ikifuatiwa na wiki mbili za kusubiria kuona kama tumeshika mimba, na halafu kuvumilia huzuni ikiwa mamba haikushika, na kuanza upya tena. (Kwa

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see:

<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

maelezo zaidi juu ya kujitunza mwenyewe wakati unapojaribu kushika mamba, tazama Sura ya 21, “Ujauzito.”)

KUTUMIA MBEGU ZA UZAZI ZA MTU MWINGINE KUFANYA UHIMILISHAJI

Kadiri wanawake wengi zaidi wasiiolewa na wenzi wasagaji wanavyoamua kupata watoto uhimilishaji kwa kutumia mbegu za uzazi za mtu mwingine anayejitolea – huingizwa kwenye uke au mji wako wa mamba – umeongezeka umaarufu. Inakadiriwa kuwa kwa nchini Marekani pekee, kati ya watoto 30,000 na 50,000 hutungwa kwa kupitia njia hii kila mwaka. (Kwa mjadala wa kina kuhusu kuamua ikiwa njia hii ya kupata ujauzito ni sahihi kwako, kumchagua mtu wa kujitolea mbegu, na kuhimilisha, tazama “Kutumia Mbegu Za Uzazi Za Mtu Mwingine Kufanya Uhimilishaji” kwenye Sura ya 25, “Kukosa Uwezo wa Kushika Mimba na Uzazi wa KUjifungua kwa Kusaidiwa.”)

KUASILI MTOTO

Kitendo cha kumuasili Katy kimekuwa faraja kubwa kuliko zote maishani mwangu. Ana umri wa miezi 11 sasa na alizaliwa huko Kazakstani. Tangu nimemuasili, watu kadhaa wamekuwa wakielezea kwa kiasi gani Katy ana bahati au jinsi gani mimi nilivyo jasiri kwa kuweza kufanya jambo hili peke yangu. Hata hivyo, ukweli ni kwamba, mimi ndiye mwenye bahati kwa kuwa na binti mzuri sana kama Katy na, ushujaa hausiani kabisa na jambo hili. Mapenzi na matamania ya kimama pekee ndivyo vimeifanya (na vinaendelea kuifanya) familia hii iwepo. Sijawahi kuwa na uhakika na jambo lolote lile na nina msisimko mkubwa sana kwamba Katy ni mwanangu kwa sasa.

AINA ZA KUASILI/KUCHUKUA MTOTO

- Katika kuasili mtoto wa ukoo mmoja au ndugu wa karibu kunajumuisha kuchukuliwa kwa mtoto kwenda kuishi na ndugu. Aina hii ya kuasili ndiyo iliyo zoeleka zaidi.

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

- Kuasili *kiserikali* kunahusisha kupewa kwa mtoto anayeasiliwa kwa wazazi wake wapya kunakofanywa na wakala wa umma, kama vile ustawi wa jamii au kitengo cha huduma za umma cha serikali. Kwa ujumla, Mwakala wa umma huwakabidhi wazazi watoto ambao wako chini ya uangalizi wa serikali kwa sababu mbalimbali kama vile baada ya kuwa wametelekezwa, wamenyanyaswa, kuachwa na wazazi na ndugu zao, au baada ya mzazi mmoja au wote wawili kuwa wamefariki. Watoto ambao kisheria bado wana muunganiko na wazazi wao wa kuwazaa wanaweza kuchukuliwa kama watoto wa kufikia, wakati wale ambao muunganiko wao kisheria na wazazi wao wa kuwazaa tayari umevunjika wanapatikana kwa ajili ya kuasiliwa.
- Kuasili *kwa binafsi* kunashughulikiwa na kampuni binafsi ya uwakala, mara nyingi mashirika ya msaada na kusaidia wenye shida au shirika la kijamii lililopewa kibali au ambalo ni la kiserikali.
- Kuasili *kwa kujitegemea* kunashughulikiwa na mtu yeyote mwingine ambaye siyo mfanyakazi wa shirika la uwakala, kama vile daktari, mwanasheria au mtu wa kati anayefanya kazi kufanikisha kuasiliwa kwa watoto.
- Baadhi ya taratibu za kuasili kwa binafsi na kwa kujitegemea *zinafanyika waziwazi*. Nyingine *haziko wazi* sana. Taratibu zilizo wazi za kuasili hujumuisha kiasi fulani cha mawasiliano kwa kipindi cha mwanzoni na/au kuendelea kuwasiliana kati ya familia inayoasili na familia ambamo mtoto anayeasiliwa amezaliwa. Wazazi halisi wa mtoto na wale wanoasili wanakubaliana juu ya wajibu wa wazazi halisi wa mtoto, mawasiliano ya baadaye, na kiwango cha uwazi kabla ya kitendo cha kuasili kufanyika. Kwa upande wa taratibu za kuasili zisizo waziwazi, si upande wa wazazi halisi wa mtoto wala ule unaoasili unaomfahamu mwenzake.
- Katika taratibu za kuasili za *ndani ya nchi*, watoto huzaliwa na kuasiliwa ndani ya nchi ya Marekani. Taratibu zote hizi zinasimamiwa na sheria za majimbo, kote katika jimbo ambamo wazazi wanaoasili wanaishi na ambamo mtoto amezaliwa.

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi ("Becoming a Parent"). For more information, see:
<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

- Kuasili *kwa kimataifa* ni utaratibu wa kuasili watoto kutoka nchi nyingine. Utaratibu huu unasimamiwa na sheria na matakwa ya kila nchi husika, pamoja na sheria za huduma za Uraia na Uhamiaji za Marekani.
- Kwa kawaida, lakini sio kila mara, wazazi wanaoasili humuasili mtoto kwenye mahakama iliyoko kwenye nchi ambamo mtoto huyo amezaliwa kabla ya kumleta mtoto Marekani. (Kwa maelezo zaidi ya kukusaidia kufanikisha mlolongo wa masharti na sheria unaoambatana na kuasili, tazama “Msaada.”)

Muda kati ya kufahamu kuwa huwezi au hupaswi kupata ujauzito na kuamua kuanza kufuata ndoto mpya ni muda unaosikitisha zaidi kuliko yote. Katika maisha hakuna uhakikisho wa kupata vitu, lakini ukielewana vizuri na shirika la uwakala wa kuasili lenye sifa nzuri, unaweza kuwa na uhakika wa kuwa mzazi. Na mara utakapokuwa umefanya uamuzi, utakuwa ni kama vile umetengeneza upinde wa mvua. Tunaiita hiimimba yetu ya makaratasi, mtoto anazaliwa mioyoni mwetu. Badala ya kukimbia maduka pale nimwonapo mwanamke mjamzito na kuepuka korido ya bidhaa za watoto kwenye soko la jumla, sasa ninatabasamu, na kuinua kichwa changu. Nina furaha isiyo kifani.

Kuasili ni njia nyingine ya kuanzisha au kupanua familia. Unaweza ukawa hauna uwezo wa kupata ujauzito, au unaweza ukawa na matatizo ya kiafya ambayo yanafanya iwe hatari kwako kubeba mamba au kujifungua. Baadhi ya wanawake wanapendelea kutobeba mamba. Wengine wanapendelea kuasili kuliko kuzaa kutokana na kuguswa na watoto wanaohitaji familia za kuwapatia mapenzi.

Kuasili kunajumuisha changamoto za kifedha, kihisia na taratibu za kumuhamishia mtoto kwenye makazi mapya. Wakati gharama, mahitaji ya mawakala wa kuasili na nchi za kigeni, au upatikanaji wa watoto wa kuasili mara nyingi hutupunguzia machaguo tunayoweza kuyafanya, kufahamu juu ya machaguo tofauti na kuwa wawazi kuhusu vikwazo vyovyote vinavyoweza kujitokeza kutasaidia kutengeneza mazingira yatakayomsaidia kila mmoja wetu.

Mimi na mwenzi wangu tulikuwepo wakati mtoto wetu wa kiume anazaliwa, kitu tunachokichukulia kama zawadi ya kipekee kwetu, baada ya kipindi kirefu sana cha kushindwa kupata mtoto na mlolongo mrefu wa kutaka kuasili mtoto. Baada ya wakati mgumu wa kujifungua, niliruhusiwa kumbeba mwanangu kwenda naye

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see:

<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

kwenye kitengo cha kinamama waliotoka kujifungua, ambapo alipimwa uzito na kufanyiwa vipimo vingine. Ilikuwa nia katika wakati huu wa pilika pilika ambapo tulikuja kubaini kuwa mama mzazi wa mwanetu alipimwa na kukutwa ameathirika na matumizi ya dawa za kulevya, na hivyo walikuwa mbioni kumpima mtoto wetu pia. Nilipatwa na hisia mchanganyiko za mkanganyiko – nilimkasirikia sana mama mzazi wa mtoto kwa kutudanganya juu ya matumizi yake ya dawa za kulevya na pia nilihofia pengine mtoto ataweza kupatwa na matatizo ambayo hatukuwa tumejiandaa kukabiliana nayo... [Mtoto] pia alionekana asiye wa kawaida – mkubwa sana na kama aliyevimba kutokana na kisukari cha mama yake ambacho hakikuwa kimetibiwa – na nilihofia kama nitaweza kumpenda mtoto ‘mbaya’ kama huyu. Kwa kipindi cha siku chache zilizofuatia, kadiri iliyokuwa inazidi kuwa wazi kuwa mama wa mtoto bado alikuwa anaendelea na msimamo wake wa kuasili, bado nilikuwa sijajua nini cha kufanya juu ya hisia zangu mchanganyiko kuhusu mtoto huyu. Cha kushangaza ni kwamba, mwenzi wangu, ambaye siku zote amekuwa akisita kuwa mzazi, ndiye alikuwa wa kwanza kuvutiwa na kumchangamkia yule mtoto. Taratibu hisia zangu zilianza kulainika zenyewe kadiri nilivyozidi kukibeba na kuongea na kitoto hiki hapo kwenye kitengo cha kinamama waliotoka kujifungua, ambapo alikaa kwa siku sita. Alianza kupungua unene na kurudia kuwa mtoto WANGU mzuri sana.

Kuna mambo kadhaa ya kuzingatia wakati unapanga kuasili mtoto. Utajisikiaje juu ya kuwa na, na kuendeleza, mawasiliano na wazazi wa kibaiolojia wa mtoto wako? Je, ungependa kuwa na mtoto ambaye anafanana na wewe kadiri inavyowezekana au unataka mtoto wa kabila tofauti au mbari nyingine kabisa? Unataka kuasili mtoto mchanga au ambaye ameshakua mkubwa kidogo? Je uko tayari kumkaribisha mtoto kwa changamoto za kihisia au kimatibabu? Uko tayari kuwa mzazi wa mtoto yeyote yule utakayefanikiwa kumuasili? Utawezaje kugharamikia mchakato mzima wa kuasili?

Inaweza kuwa jambo la busara kupata jumuiya ya wazazi wanaotegemea kuasili, au ambao tayari wameasili mtoto/watoto. Wanaweza kujibu aswali uliyonayo, kukuelekeza namna ya kupata msaada na kuwa pamoja nawe katika furaha na mifadhaiko inayotokana na mchakato wa kuasili mtoto. Vikundi hivi vinapatikana kwenye majiji mengi, na tovuti nyingi zinazohusika na kuasili watoto zinatoa msaada wa moja kwa moja kupitia kwenye mtandao.

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

GHARAMA

Kuasili mtoto mara nyingi huwa ni mchakato wenye gharama kubwa. Ili kusaidia kupunguza gharama, serikali kuu huwapatia familia zilizoasili pendeleo la kodi la mpaka dola 10,160 kwa mtoto; majimbo mengi pia hutoa upendeleo au makato ya kodi. Jeshi nalo hurudisha sehemu ya gharama kwa familia zilizoasili watoto.

Mikopo yenye riba kidogo au isiyo na riba kabisa pia inapatikana maalaumu kwa familia zilizoasili, na waajiri wengi siku hizi wanatoa manufaa ya kuasili mtoto. (Kwa maelezo kuhusu kugharamikia mchakato wa kuasili mtoto na kuwapata waajiri wanaotoa manufaa ya kuasili mtoto, tazama “Msaada.”)

“NA WAKANIKABIDHI JESSICA”

RACHEL GINGOLD

Sikuweza kuamini. Wazazi wote hawa wa Kimarekani wakiwa na kamera zao, na walezi wote hawa wa kichina wakikutana kwenye chumba cha mikutano kwenye hoteli jimboni Fujian, nchini China. Watoto hawa wachanga walikuwa wanalia, na wazazi wao pia nao walikuwa wakilia. Ilikuwa ni kelele kila mahali, lakini pia ilikuwa inahuzunisha. Halafu mara mtu akatokea, akaita majina yetu, na wakamkabidhi Jessica kwangu. Nkafikiria, Mungu wangu! Ninataka kufanya nini? Huyu hapa ni mwanangu, nimembeba mikononi mwangu. Mimi ndiye mama wa mtoto huyu kwa sasa. Licha ya kwamba ilinichukua zaid ya mwaka kufanya mpango na kujaza kila aina ya fomu katika kufanikisha kumuasili mtoto huyu, bado kitendo kilionekana cha kushtukiza sana. Nilikuwa na hofu: Atakubali? Atapiga makelele sana? Je, ana afya njema?

Basi nikkamchukua na kumpeleka kukutana na baba yake pamoja na dada yake mpya (ambaye pia aliasiliwa kutoka China), na Jessica alionekana mwenye kuduwaa kidogo pia. Kwa siku kadhaa za mwanzo alikuwa hataki kubanduka mikononi mwangu, lakini baada ya kufahamu kuwa wote tutammtunza vizuri, akaanza kutuchangamkia wote.

Watu wengi nchini China wanapendelea watoto wa kiume, na mtu unaweza kuwa na mtoto mmoja au wawili pekee. Kwa kuwa hakuna sera inayoweza

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see:

<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

kuwaruhusu watu kutoa watoto wao kwa ajili ya kuasiliwa, watu hulazimika kuwatelekeza. Kuna watoto wengi sana wa kike waliotelekezwa. Ni tatizo linaloumiza moyo.

Sote tunavutiwa na utamaduni wa Kichina. Na sote pia tunategemea kuanza kujifunza lugha ya Kimandarin na, watakapokuwa wakubwa, tuwapeleke tena China. Watu wana hamu ya kufahamu zaudu kuhusu sisi na wana maswali mengi ya kutuuliza kwa sababu hatufanani na familia nyingine, lakini tuna bahati ya kuishi kwenye jumuiya yenye mchanganyiko wa tamaduni tofauti.

MAMBO YA KUZINGATIA KIMAADILI WAKATI WA KUASILI MTOTO

Mchakato wa kuasili unaweza kutulazimisha kukabiliana na maswali magumu ya kimaadili ambayo ni nadra sana kufikiriwa na wale wanaopata watoto kwa kujifungua kwa njia ya kawaida. Kwa nini mafunzo ya nyumbani na hatua nyinginezo za kuwafanya wazazi wawe imara katika malezi yanaachwa kutolewa pekee kwa wale wanaoasili? Ni udhibiti kiasigani tunatakiwa tupewe juu ya uchaguzi wa mtoto. Tutawezaje kufahamu, kuepuka, na kufanya juhudi kukunga mazingira ambayo yanaweza kuwafanya wazazi wa kibaiolojia wa watoto wanaoasiliwa wasijisikie kunyonywa na kuonewa? t

Unawezaje kudumisha uwiano kati ya uwezekano wa uwepo wa mahitaji tofauti ya mtoto, wazazi wa kumzaa, na wazazi wa kumasili kuhusu kiwango cha kuwa wazazi katika kuasili? Je, kwa wale miongoni mwetu tunaoishi kwenye mataifa *tajiri* “tuna wajibu’ wa kuwatunza watoto waliochwa bila makazi au walio katika mazingira magumu sehemu nyingine duniani kutokana na umasikini au unyanyasaji mwingine uaofanyika kwenye jamii? Tutawezaje kuwasaidia watoto weti kukabiliana na masuala ya kimbari, kitamaduni, na utambulisho tunayoweza kukumbana nayo?

Kwa majadiliano zaidi juu ya maswali ya kisiasa, kijamii, kimbari, na kiuchumi, tazama “Masuala ya Kimaadili katika Kuasili” [W40] kwenye tovuti, www.ourbodiesourselves.org).

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

HISIA NA MAHUSIANO

Mchakato wa kuasili mtoto unaweza kuwa safari ya kihisia. Ni jambo la kufurahisha kuwapokea watoto wetu, lakini pia kuna nyakati tunajisikia kufadhaika, huzuni, kotokuwa na nguvu au uwezo wowote, hofu, na kutokuwa na subira. Endapo ulikuwa hauna uwezo wa kushika mamba, unaweza kugundua kuwa kuasili mtoto hakukufanyi ujisikie nafuu yoyote. Unaweza kufurahia kwamba hatimaye utaitwa mama, lakini bado ukaendelea kuhuzunikia ujauzito ambao kamwe hautoupata.

Ikiwa umefanya uamuzi wa kuasili kwa kuwa umechagua au umependelea kufanya hivyo na si kwa sababu hauna uwezo wa kushika mimba, mambo ya msingi utakayokabiliana nayo yanaweza kuwa ni kufanikiwa kumpata na hatimaye kumchukua mtoto wako. Muda utakaoutumia kumpata mtoto wako unaweza ukauona mrefu sana, na ni vigumu kupangilia mambo mapema.

Wanawake wanaoingia kwenye kundi la wazazi kwa kupitia njia ya kuasili mtoto wanahitaji msaada kama vile ilivyo kwa wanawake ambao ni wajawazito . Utaratibu wa maisha yako, kujitambua kwako, na mahusiano yako yatabadilishwa pia – au zaidi kuliko – ikiwa ulikuwa unapanga kubeba ujauzito. Zaidi ya hapo, unaweza kukabiliwa na changamoto za kipekee zinazoambatana na mchakato mzima wa kuasili mtoto. *Hautoonekana* kuwa mjamzito, hivyo unaweza kuchagua kujadili kiundani mchakato mzima wa kuasili. Kwa upande mwingine, baadhi ya watu wanaweza kuutilia shaka uzoefu wako wa kwa kuwa hawaoni uko kwenye mchakato wa kuwa mzazi. Vilevile, kuna baadhi ya watu bado wanalichukulia suala la kuasili kwa mtazamo usiofaa na hawakubaliani nalo.

FAMILIA NA WAZAZI WANAHITAJI KUSAIDIWA SANA

Kuwa mzazi ni shughuli pevu, kihisia na kimwili. Jamii yetu iendayo kasi na inayoongozwa na teknolojia haishughulikii mahitaji changamani ya wazazi na watoto, na wala haisaidii wala kujali utoaji wa huduma ndani ya familia. Ili wanawake waweze kudumisha uwiano kati ya mahitaji ya kifamilia na kazi, jamii kwa ujumla inahitajika kuwa tayari kukubali maamuzi magumu kuhusu sera za kifamilia ambazo zinatoa kipaumbele kwa mahitaji ya wanawake na watoto.

Sheria ya mapumziko ya kifamilia na kwa ajili ya matibabu ya mwaka 1993 inaagiza kuwa makampuni yenye waajiriwa hamsini au zaidi kuwaruhusu wafanyakazi kurudi makazini kwa kiwango sawa baada ya kuwa kwenye

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi (“Becoming a Parent”). For more information, see:

<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

mapumziko ya kuihudumia familia. Lakini bado wanawake wengi wanafanya kazi kwenye makampuni madogo madogo; na zaidi ya hapo mapumziko ya lazima ya kwa ajili ya kujifungua hayana malipo. Baadhi ya mabadiliko yako njiani kufanyika. Kuanzia Julai mwaka 2004, jimbo a California lilipanua zaidi sheria hii ya Serikali kuu ya Mapumziko ya Kifamilia na Kimatibabu ili kuwawezesha waajiriwa wa kampuni ya ukubwa wowote iliyopo jimboni humo kupata sehemu ya malipo kwa kipindi cha mpaka wiki sita (kwa wakati chochote ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili) ili kuwezesha matunzo ya mtoto aliyezaliwa au mwanafamilia anayeumwa. Tunahitaji sera kama hizi kila mahali nchi nzima. Wafanyakazi wote wanahitaji likizo za uzazi zenye malipo pamoja na ulinzi wa kazi kwa wazazi; kurudi kazini taratibu bila adhabu zozote; huduma nafuu zenye ubora za matunzo ya kila siku; programu maalumu za kuwawezesha kurudi tena makazini wazazi waliochukua likizo kuwalea watoto wao zitakazotolewa kwa kwango sawa; likizo ya wazazi pale watoto wanapokuwa wagonjwa; na muda wa ziada na mfumo wa kuwaruhusu wafanyakazi kufanya kazi kwa muda na, kwenye maeneo maalumu ya kupangiwa, pamoja na machaguo ya kuweza kufanya kazi kwa kushirikiana.

Kulea watoto ni kazi ya muhimu na ya thamani inayostahili msaada wa kijamii na kiuchumi pia. Kwa vyovyote vile, sisi binafsi – iwe tumechagua kuwa na watoto au la, tuna wajibu wa kipekee kwa kizazi kijacho na lazima tufanye kazi kwa pamoja kuinua ubora wa sera zinazohusu kifamilia.

FAMILIA ZA WAZAZI WASAAGAJI NA KUASILI

Wakati idadi inayoongezeka ya wasagaji, watu wenye jinsia mbili na wanawake waliobadilisha jinsia wanachagua kuasili watoto, wengi wetu bado tunakumbana na unyanyasaji kadiri tunapokuwa tukipanua familia zetu. Ingawa makampuni mengi ya uwakala wa kuasili watoto yako tayari kushirikiana waziwazi na wasagaji walio waseja au waliooana katika kuasili mtoto, wetu hulazimishwa kuasili tukiwa kama kina mama waseja wasio na kasoro yoyote ya ujinsia. Hata hivyo, mara tu baada ya mchakato wa kuasili kukamilika, majimbo mengi yanatoa fursa ya watu wa jinsia moja kutambuliwa kisheria kama wazazi kupitia kuasili kwa mzazi wa pili.

Tovuti ya Kampeni ya haki za Binadamu (*The human Rights Campaign – HRC*) (www.hrc.org) ina taarifa za kina zaidi kuhusu maamuzi na masuala ya kisheria maalumu yanayowakabili wanawake wasagaji na wa jinsia zote mbili walio katika mchakato wa kuasili mtoto. Taasisi hii pia inatoa huduma ya kutunza tarifa

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi ("Becoming a Parent"). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>

zote kwa ajili ya kukusaidia kutafuta makampuni ya uwakala wa kuasili yasiyo na masharti magumu.

Machaguo Ya Uzazi Kufikiria Kuwa Mzazi ("Becoming a Parent"). For more information, see:
<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>